PJ PROJECTS Suluhisho La Mjasiriamali. 0659908078 | 0754745798

PJ PROJECTS **“Suluhisho La Mjasiriamali”**

Tel +255754745798 / +255659908078 Mwanza-Tanzania

# JINSI YA KUTENGENEZA CHAKI KWA KUTUMIA CLAMP MOULD

Tunapatikana kwenye mitandao ya jamii;

Facebook page: **@think Big Start Small**

YouTube**:@pjprojects**

Website: **www.piusjustus.com**

Emai: **piusjustus28@gmail.com**

Whatsapp: **+255754745798 / +255659908078**

**HATUA ZA UTENGENEZAJI**:

Fungua mashine na uioshe kwanza kwa maji na sabuni kama ni kwa mara ya kwanza inatumika. Suuza vizuri na maji masafi na uiache ikauke vizuri.

1. Funga mashine kwa usahihi kwa kufuatana na namba zilizoko kwenye mashine (in ascending order) na unganisha matundu kwa nguvu kwa kutumia kifungio kilichopo kwenye mashine.
2. Laininsha mashine kwa kutumia brush ya kawaida ya kupakia rangi kwa mafuta ya kula yaliyochanganywa kwa mafuta ya taa kwa uwiano wa 1:1 (Maelekezo yanapatikana kwenye kitabu, unaweza kuagiza kutoka kwenye manual/e-book tukakutumia kupitia whatsapp yako kwa gharama ya Tsh. 10,000/- tu tupigia au whatsapp +255754745798)
3. Weka kitambaa kizito chini ya mashine, hii hutumika kuzuia uji wa chaki utakaowekwa kwenye mashine usisambae kutoka kwenye matundu ya mashine.
4. Changanya mchanganyiko wa malighafi kwa usahihi kwa uwiano wa 1:1 kisha mwaga juu ya mashine kwa kujaza matundu yote yaliyopo kwenye

mashine ya chaki. Ukishajaza, acha kwa muda kabla ya kukwangua juu ili mchanganyiko uingia vizuri kwenye matundu ya mashine.

5. Wakati wa kumwaga mchanganyiko huo kwenye mashine, anzia matundu yaliyoko katikati mwa mashine huku ukienda kwenye matundu ya pembeni, hii husaidia uji kutomwagika sana pembeni mwa mashine. Fanya hivi kwa uharaka kwani uji unaweza kuganda kabla ya kumaliza.
6. Acha mchanganyiko wako ukae kwa dakika tano kwenye mashine, baada ya hapo unaweza kukwangua juu na chini ya mashine ili sehemu hizo ziwe flat kabisa (kuondoa mabaki ya uji uliozidi). Fanya hivi kwa kutumia screpa ya bati au plastic.
7. Kisha endelea kusubiri kwa muda wa dakika 10 ili chaki ziweze kuwa ngumu zaidi ndani ya matundu ya mashine.
8. Sasa unaweza kufungua mashine kwa ajili ya kutoa chaki zilizotengenezwa ndani ya matundu. Fungua kwa umakini ili chaki zisivunjike. Ondoa chaki moja baada ya nyingine kwa kusukuma juu ya chaki kwenye chini au chini kwenda juu kisha inyanyue kuitoa. Fanya hivi kwa umakini kuzuia chaki kuvunjika vunjika.
9. Hamisha chaki kwenda kwenye jua ili kukausha vizuri, au tumia solar dryer. Rudia hatua hizi kila siku mpaka chaki zikauke vizuri.
10. Fungasha chaki kwenye box lililoko tayari kwa ajili ya mauzo.

**NOTE**: Mashine hizi ni nzuri sana kwa mtu anayeanza mradi huu, lakini kwa mtu ambaye ameamua kuwekeza nguvu zake katika mradi huu, tunamshauri aanze kuwekeza pesa kwa ajili ya kupata mashine kubwa itakayomzalishia chaki nyingi na bora kwa wakati mfupi sana. Mashine hizo ni kama **(IMM machine)**. Unaweza kupata kuzifahamu mashine hizi katika kurasa zetu za kijamii @Think Big Start Small au unaweza kuwasiliana nasi whatsapp **+255754745798 / +255659908078** tutakupatia ufafanuzi zaidi.

**<u>AINA ZA MASHINE</u>**




